



Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 APRILI, 2021 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 21-30 APRILI, 2021.

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 APRILI, 2021.

Kipindi hiki kilitawaliwa na kudhoofika kwa migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo la Kaskazini (Azore na Siberia) pamoja na kuimarika kwa migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo Kusini (St. Helena na Mascarene). Hali hii ilisababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kusukumwa kidogo kuelekea upande wa Kaskazini mwa nchi yetu na hivyo kuendelea kutoa mchango katika utengenezaji wa mvua katika maeneo hayo. Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani liliendelea kuwepo katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi, hali iliyoendelea kutoa mchango wa kutokea kwa migandamizo midogo ya hewa katika eneo hilo. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani liliendelea kuwepo eneo la kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) na hivyo kuendelea kuleta mchango hafifu katika kusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea katika maeneo ya magharibi mwa nchi yetu.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 APRILI, 2021.

Mifumo ya hali ya hewa iliyotajwa hapo juu ilikua na mchango katika kuwepo kwa vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya ukanda wa ziwa Victoria pamoja na maeneo ya mwambao wa pwani. Hata hivyo, vipindi vifupi vya mvua zilizoambatana na ngurumo vilijitokeza katika meneo machache Magharibi, Kusini pamoja na nyanda za juu kusini-magharibi mwa nchi. Maeneo ya nyanda za juu kaskazini-mashariki pamoja na kati mwa nchi yaliendelea kupata vipindi vya mvua katika maeneo machache.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21- 30 APRILI, 2021.

2.1 VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 21-30 APRILI, 2021

Katika dekadhi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo la Kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika, wakati ile iliyopo eneo la Kusini (St. Helena na

Kwa Mawasiliano:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S. L. P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukandamvua (ITCZ) kusalia katika maeneo ya Kaskazini mwa nchi yetu. Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi. Hali ambayo inatarajiwa kuleta mchango wa uwepo wa migandamizo midogo ya hewa kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi. Aidha upande wa kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) joto la bahari linatarajiwa kuwa juu kidogo ya wastani. Hali hii haitarajiwi kuwa na mchango mkubwa katika mifumo ya hali ya hewa inayosukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka mistitu ya Congo kuelekea katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 21-30 APRILI, 2021.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua na ngurumo.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua katika maeneo machache.

Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya Kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua na ngurumo katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua na ngurumo katika maeneo machache.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa na vipindi vichache vya mvua.

Nyanda za juu Kusini-Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa na vipindi vichache vya mvua katika maeneo machache.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

Imetolewa na:

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.

Kwa Mawasiliano:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S. L. P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

727F -00/2019